# TUMAINI DISTRICT HOSPITAL

## KUSAIDIWA KUJIFUNGUA KWA NJIA YA VACUUM ASSISTED BIRTH (VAB)

**VAB** : Ni njia salama ya kujifungua kwa kawaida ambapo mama atasaidiwa kumtoa mtoto kwa kifaa maalumu kiitwacho Vacuum machine.



Kifaa iki kitawekwa kwenye ngozi ya kichwa cha mtoto na mkunga(mtoa huduma wa afya)wenye ujuzi na uzoefu atamsaidia mama kumtoa mtoto kwa kufuata muongozo.



**IMETHIBITISHWA NA SHIRIKA LA AFYA DUNIANI PAMOJA NA WIZARA YA AFYA TANZANIA**
**NI SALAMA KWA MAMA NA MTOTO NA WENGI WAMESAIDIWA KWA NJIA HII**

## NANI ANAWEZA KUSAIDIWA KUJIFUNGUA NA VAB

- Mjamzito yoyote ambaye anauchungu na amekaribia
- kujifungua na amekidhi vigezo kutokana na
- uchunguzi wa watoa huduma



## MAMBO YANAYOHITAJIKA KUTOKA KWA MJAMZITO NA NDUGU/MUME

- Kuelewa faida na hasara za hii njia
- Kutoa au kutokutoa ridhaaya kusaidiwa kwa hii njia
- Kutoa ushirikiano wakati kusaidiwa kwa njia hii kwa
- kadri ya maelekezo ya mtoa huduma



## FAIDA ZA VAB

- Inazuia kukaa kwenye uchungu kwa muda mrefu wakati mtoto amekaribia kutoka
- Haiongezi gharama za matibabu
- Inamuepusha mama na upasuaji usio wa lazima
- Inamuepusha mtoto kukaa kwenye njia kwa muda mrefu na kuumia ubongo kwa kukosa oksijen
  Mama kupona haraka baada ya uzazi na kurudi kwenye shughuli zake za kawaida ndani ya muda mfupi

## MADHARA YA KUJIFUNGUA KWA NJIA YA VAB

- Mama kuchanika njia.
  hii ikitokea watoa huduma watamshona mama kama ilivyo wakati wa kujifungua kawaida.
- Kuvimba ngozi ya kichwa cha mtoto.
  hii hali itaisha yenyewe baada ya siku chache haitaji matibabu yoyote.

**Tumaini Vab TOT**
**Contact Us**
**Halima Chande:+255 620 243 951**
**Petrolina Mao +255 767 758 142**